AFRICAN UNION

الاتحاد الأفريقي

UMOJA WA AFRIKA

UNION AFRICAINE

UNIÃO AFRICANA

UNIÓN AFRICANA



Addis Ababa, Ethiopia P. O. Box 3243 Telephone: +251 115 517 700 Fax: +251 115 517 844
Website: www.au.int


**BARAZA KUU**
**Kikao cha Kawaida cha Arobaini na nne**
**14 - 15 Februari 2024**
**Addis Ababa (Ethiopia)**

**EX.CL/1517(XLIV)**
Matini Chanzi: Kingereza

# RIPOTI YA KAMATI YA MAWAZIRI YA UFUATILIAJI JUU YA UTEKELEZAJI WA AJENDA 2063

AFRICAN UNION | UNION AFRICAINE

الاتحاد الأفريقي | UNIÃO AFRICANA

UMOJA WA AFRIKA | UNIÓN AFRICANA

Addis Ababa, ETHIOPIA P.O. Box 3243 Telephone: +251-115-517 700 Fax: +251-115517844
website: www. africa-union.org


**RIPOTI YA MKUTANO WA KAMATI YA MAWAZIRI YA UFUATILIAJI WA AJENDA 2063**
**9 Februari 2024**
**Kwa njia ya mtandao**

# RIPOTI

## A. UTANGULIZI

1. Mkutano wa Kamati ya Mawaziri ya Ufuatiliaji wa Ajenda 2063 uliongozwa na Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kanda wa Jamhuri ya Ghana. Mhe Shirley Ayorkor Botchwey.

Wajumbe waliohudhuria

i. Ghana
ii. Libya
iii. Rwanda
iv. Burundi
v. Namibia
vi. Senegal
vii. Comoro
viii. Angola
ix. COMESA
x. SADC
xi. IGAD
xii. CDCP
xiii. UNECA
xiv. ACBF

## B. UFUNGUZI WA MKUTANO

2. Mwenyekiti wa Kamati ya Mawaziri kuhusu Ajenda ya 2063, **Mhe. Shirley AyorkorBotchway, Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kanda**, alifungua kwa kuwakaribisha wajumbe wote wa kamati kwenye mkutano na kuwashukuru kwa kuhudhuria. Kisha akatoa wito wa kukaa kimya kwa muda ili kumkumbuka Mhe. Rais Hage Geingob.

3. Kuhusu masuala ya msingi ya kujadiliwa, alidokeza kuwa mkutano huo ungejikita kwenye majukumu manne ya kimkakati ya kamati, ambayo ni pamoja na kutoa mwongozo wa kimkakati, kuhakikisha utekelezaji mzuri, ufadhili na uwajibikaji katika utekelezaji wa Ajenda 2063. Alisisitiza umuhimu wa kuhakikisha. ushirikishwaji na ujumuishwaji katika Ajenda 2063, kwa kuzingatia umuhimu wa mchango wa wananchi wa bara hili, hususani wanawake na vijana katika kutimiza maono yake.

4. Alishukuru kwa kazi ya Kikosi Kazi cha Kitaalamu, hasa, mwongozo na uongozi wa Mkurugenzi wa Mipango Mikakati na Utekelezaji na akamalizia kwa kutoa hakikisho la Mwongozo wa Kimkakati ambao Kamati itatoa kwa Ajenda 2063.

5. Makamu Mwenyekiti (DCP) wa Kamisheni ya Umoja wa Afrika, Mhe, Dkt Monique Nsanzabaganwa, katika hotuba yake ya ufunguzi, **alitoa salamu za rambirambi** kwa watu wa Namibia kufuatia kifo cha Rais Hage Geingob.

6. DCP iliipongeza Kamati ya Mabalozi iliyomaliza muda wake na Kikosi Kazi cha Kitaalamu cha UA kuhusu Ajenda ya 2063. Alisisitiza kwamba Ajenda ni wito wa kuchukua hatua kwa wananchi wote, taasisi na marafiki wa Afrika katika ngazi zote kuchangia katika "Afrika tunayoitaka". DCP alisisitiza umuhimu wa kuimarisha

uratibu, ufuatiliaji, tathmini na utoaji taarifa, pamoja na kuboresha usimamizi wa data na uwezo wa takwimu. Alisisitiza haja ya kukuza ushirikiano ili kuongeza ufanisi wa matokeo. Alibainisha dhamira ya uongozi wa UA kufanya kazi na Kamati ya Mawaziri ya Ufuatiliaji ili kutoa mwongozo wa kimkakati kuhusu Ajenda.

**C. Ajenda**

i. Kufungua Mkutano
ii. Kupitishwa kwa Rasimu ya Ajenda
iii. Kuwasilisha na kujadili Ripoti ya Kamati ya Mabalozi ya Ufuatiliaji kuhusu Utekelezaji wa Ajenda 2063.
iv. Majadiliano
v. Kujadili rasimu ya Uamuzi
vi. Mengineyo na
vii. Kufunga Mkutano

7. Ajenda zilipitishwa kama zilivyowasilishwa

**D. Kuwasilisha na kujadili Ripoti ya Kamati ya Mabalozi ya Ufuatiliaji kuhusu Utekelezaji wa Ajenda ya 2063.**

8. Mhe. Amma AdomaaTwum-Amoah, Balozi wa Jamhuri ya Ghana, aliwasilisha ripoti ya Mkutano wa Kamati ya Mabalozi uliofanyika kuanzia tarehe 5 – 7 Februari na kuhudhuriwa na nchi za Ghana, Namibia, Burundi, Senegal, Comoro na Cote d'Ivoire (Kinara wa Ajenda 2063).

9. Aliufahamisha mkutano kuhusu mada zilizowasilishwa kwa Kamati ya Mabalozi wakati wa mkutano wake wa kutathmini mikutano mbalimbali vya kitaalamu na uthibitisho iliyofanyika tangu mkutano wa mwisho cha Mabalozi. Mawasilisho hayo pia yaliijulisha Kamati kuhusu maboresho yaliyofanywa kwenye Ripoti ya Tathmini ya FTYIP na rasimu ya STYIP. Mawasilisho hayo yalijumuisha:

i) Taarifa kuhusu Mradi Maalumu
ii) Ripoti ya Tathmini ya FTYIP ya Ajenda 2063
iii) Rasimu ya Mpango wa Pili wa Utekelezaji wa Miaka Kumi (2024 – 2033)
iv) Vichocheo vya Mpango wa Pili wa Utekelezaji wa Miaka Kumi

10. Balozi aliujulisha mkutano huo kuhusu mapendekezo yaliyotolewa baada ya majadiliano shirikishi katika kila moja ya mawasilisho yaliyotajwa hapo juu.

11. Mkutano huo pia uliarifiwa kuhusu mawasilisho ya ziada yaliyofanywa kuhusu Hadidu za Rejea za Kamati ya Mawaziri na Mpango Kazi wa Mwaka wa Kamati ya Mawaziri.

12. Baada ya maombi ya ufafanuzi, ilifafanuliwa kwamba Mkutano Maalumu wa Wakuu wa Nchi na Serikali hautamaanisha kufutwa kwa Uzinduzi utakaofanyika wakati wa mkutano huo mwezi Februari 2024. Ilielezwa kuwa Mkutano wa wakuu wa Nchi na Serikali wa Februari ulikusudiwa kuongeza ushiriki wa Wakuu wa Nchi kwenye STYIP kwa ajili ya kuongeza umiliki na mwonekano katika bara zima.

13. Kisha mkutano ulipitisha ripoti ya Kamati ya Mabalozi ikijumuisha mapendekezo.

**E. Kujadili rasimu ya Uamuzi wa Ajenda2063.**

14. Rasimu ya Uamuzi kuhusu Ajenda 2063 iliwasilishwa kwenye mkutano. Mkutano huo uliomba kuboreshwa kwa maudhui ya Uamuzi wa Mkutano Maalumu wa Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali kwa ajili ya kueleweka kwa urahisi. Uamuzi wa kuzitaka RECs kutoa taarifa ya maendeleo ya utekelezaji wa Ajenda 2063 STYIP wakati wa Mikutano ya Uratibu wa Nusu Mwaka ulirekebishwa. Rasimu ya Uamuzi huo ilipitishwa na pamoja na marekebisho.

**F. Kufunga Mkutano wa Kamati ya Mawaziri ya Ufuatiliaji**

15. Makamu Mwenyekiti alitoa shukurani kwa Mwenyekiti kwa uongozi wake na wajumbe wa Kamati ya Mawaziri huku akibainisha hatua kubwa ya kuanzishwa kwa STYIP na kuwataka wadau wote muhimu kuuwezesha mfumo ili kutekeleza, kufuatilia na kutoa taarifa za STYIP. Aidha alimshukuru Kinara wa UA kwa kuendelea kusaidia na kutoa mwongozo.

16. Hatimaye, Mwenyekiti wa Kamati ya Mawaziri aliwapongeza wajumbe wote na kubainisha mafanikio makubwa yaliyopatikana kwenye STYIP kuidhinishwa na kuzinduliwa wakati wa Mkutano huo Februari 2024.

**RASIMU YA UAMUZI**
**WA KAMATI YA MAWAZIRI YA UFUATILIAJI KUHUSU AJENDA 2063**
**KUHUSIANA NA MRADI MAALUMU NA UZINDUZI WA STYIP**

**Baraza Kuu,**

1. **LINAREJELEA** Uamuzi wa Baraza Kuu **EX.CL/Dec.1164(XL)** ambao uliitaka Kamisheni ya Umoja wa Afrika (AUC), na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Afrika (AUDA-NEPAD) kuongoza mchakato wa tathmini ya Ajenda 2063 FTYIP (2014). - 2023) na maendeleo ya STYIP (2024-2033), ambayo pia inajulikana kama "Mradi Maalumu".

2. **LINAKIPONGEZA** Kikosi Kazi cha Kitaalamu (AUC, AUDA-NEPAD, APRM, ACBF, UNECA na UNICEF) kwa utekelezaji mzuri wa "Mradi Maalumu", kwa kutambua uungwaji mkono usioyumba wa Nchi Wanachama, Jumuiya za Kiuchumi za Kanda, timu ya kitaalamu ya Kinara wa Ajenda 2063, Taasisi zingine za AU, UNDP, na Mashirika mengine ya Umoja wa Mataifa, Benki ya Maendeleo ya Afrika na wabia wengine wa Maendeleo kwa michango ya kitaalamu na kifedha katika kufanikisha utekelezaji wa Mradi Maalumu.

3. **LINAPITISHA** Ripoti ya Tathmini ya Mpango wa Utekelezaji wa Miaka Kumi ya Kwanza (2014 – 2023) wa Ajenda 2063 na mapendekezo yaliyomo.

4. **LINAPITISHA** Mpango wa Pili wa Utekelezaji wa Miaka Kumi (STYIP) wa Ajenda 2063 na **LINAPENDEKEZA** kuwa Mpango huo uzinduliwe kama mwongozo wa Afrika wa kuharakisha maendeleo endelevu katika muongo ujao (2024 - 2033).

5. **LINAPENDEKEZA** kwamba Mkutano Maalumu wa Uzinduzi wa Ajenda 2063 STYIP unapaswa ufanyike ifikapo Desemba 2024. Mkutano huo unapaswa kuandaliwa na Kinara wa Ajenda 2063, Mhe. Rais wa Cote d'ivoire. Unapaswa kuwa shirikishi zaidi ili kuongeza uelewa na kuongeza mwonekano wa Ajenda katika ngazi zote za utekelezaji.

6. **LINAIOMBA** Kamisheni ya Umoja wa Afrika (AUC) kuimarisha uratibu wa jumla wa vyombo ndani na nje ya UA; Nchi Wanachama, Jumuiya za Kiuchumi za Kanda, Taasisi za UA, Wabia wa Afrika wa Kitaalamu na Maendeleo, Taasisi za Kifedha za Afrika na wabia wengine wa Kimataifa wanaoshirikiana kwa ajili ya utekelezaji bora wa Ajenda 2063 STYIP.

7. **LINAOMBA** kuongezwa muda wa Mradi Maalumu wa AUC kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Afrika (AUDA-NEPAD) ili kuitekeleza ndani ya nchi, kujenga uwezo, kusimamia na kuratibu utendaji kazi na kutoa taarifa kuhusu Ajenda 2063. Aidha, **LINAZIAGIZA** AUC na AUDA- NEPAD, kwa ushirikiano na taasisi zinazohusika za Afrika zenye jukumu la kupata ufadhili wa Ajenda 2063, ili kukamilisha kazi ya Mfuko wa Maendeleo ya Ajenda 2063 na kuiwasilisha ili kujadiliwa na Kamati ya Mawaziri kuhusu Ajenda 2063 miongoni mwa vyombo vingine.

8. **LINATOA WITO KWA** Umoja wa Afrika kutenga rasilimali za kutosha kwa ajili ya uratibu wenye ufanisi, kujenga uelewa, kutekeleza ndani ya nchi na kujenga uwezo wa Nchi Wanachama kuhusu Ajenda 2063 STYIP.

9. **LINAVIAGIZA** vyombo vyote vya UA, kwa mujibu wa mamlaka na sheria zao, kutekeleza maamuzi ya awali yanayohusiana na Ajenda 2063 na kuharakisha utekelezaji wa muongo wa pili wa Ajenda 2063.

10. **LINAKUMBUSHA** mamlaka ya kamati ya Mawaziri ya ufuatiliaji kuhusu utekelezaji wa Ajenda 2063 **Ex.CL/Dec.807(XXIV)** kutoa mwelekeo wa kimkakati wa programu maalumu ili kuoanisha na kutekeleza ili kuelekea muongo wa pili wa malengo na vipaumbele vya Ajenda 2063. Kamati pia inapaswa kufanya usimamizi wa ufuatiliaji na utoaji wa taarifa za mara kwa mara.

11. **LINAIAGIZA** Kamisheni kuratibu pamoja na RECs ili kujumuisha Ajenda 2063 kama kipengele katika ripoti ya RECs kwenye Mkutano wa Uratibu wa Nusu Mwaka wa Kamati za Uchumi za Kanda (RECs) kuhusu utekelezaji wa mkutano huo.

12. **LINAPENDEKEZA** kuwa Nchi Wanachama zifikirie kuridhia kuanzisha Taasisi za Kifedha, hasa Benki ya Uwekezaji ya Afrika, kama sehemu kuu ya Ajenda ya 2063 ya ufadhili.

13. **LINATOA WITO** KWA Vyombo vya UA, Nchi Wanachama na Jumuiya za Kiuchumi za Kanda kuoanisha mipango yao ya maendeleo na Mpango wa Pili wa Utekelezaji wa Miaka Kumi (STYIP) wa Ajenda 2063.

14. **LINATOA WITO KWA** Wabia wa Maendeleo - ikiwa ni pamoja na Mashirika ya Umoja wa Mataifa kuoanisha mikakati yao na ushirikiano wao ili kuiunga mkono Afrika kwenye Mpango wa Pili wa Utekelezaji wa Miaka Kumi (STYIP) wa Ajenda ya 2063.

**AFRICAN UNION UNION AFRICAINE**

**African Union Common Repository** **http://archives.au.int**

Organs Council of Ministers & Executive Council Collection

2024-01-15

# Report of the Ministerial Follow-up Committee on the Implementation of Agenda 2063

African Union

African Union

https://archives.au.int/handle/123456789/10547

*Downloaded from African Union Common Repository*